



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA
BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



UTARATIBU WA KUFANYA MAOMBI YA MAREKEBISHO YA MAJINA

1.0 UTANGULIZI

Baraza la Mitihani la Tanzania hushughulikia maombi ya marekebisho ya majina ya watahiniwa yaliyokosewa kuandikwa katika mitihani ya Shule za Msingi, Sekondari na Vyuu vya Ualimu. Ufuatao ni utaratibu unaotumika katika kuwasilisha maombi na kufanya marekebisho.

2.0 MASHARTI YA MAREKEBISHO YA MAJINA

- (a) Maombi ya marekebisho yawasilishwe katika kipindi kisichozidi mwaka mmoja baada ya matokeo ya mtihani kutolewa.
- (b) Jina linalotakiwa kufanyiwa marekebisho ni lazima liwe linatofautiana na Jina lililotumika katika mtihani wa sifa iliyomuwezesha kusajiliwa. Hivyo lengo la marekebisho ni kufanya jina lifanane na jina lililotumika katika mtihani wa sifa.
- (c) Marekebisho yanayolenga **kuongeza jina jipya** au **kuondoa/kubadilisha jina** hayaruhusiwi.
- (d) Msingi pekee wa marekebisho ya majina ni jina la mtahiniwa lililoandikwa katika mtihani wa sifa na sio jina lililopo katika viapo vya mahakamani, vyeti vya kuzaliwa, vyeti vya ndoa, ubatizo n.k.

3.0 HATUA ZA KUFUATA WAKATI WA KUFANYA MAOMBI

- (a) Maombi yanayoshughulikiwa na shule, Mkuu wa shule/Mwalimu Mkuu ajaze fomu ya marekebisho au 'Query Circular Form' inayobainisha kosa lililofanyika katika jina na jina sahihi linavyotakiwa kuandikwa.
- (b) Maombi yanayoshughulikiwa na mzazi/mtahiniwa; ajaze fomu ya marekebisho ya jina inayopatikana katika tovuti ya Baraza la Mitihani.
- (c) Lipia ada ya marekebisho ya jina ya sh.**35,000/=** (kwa cheti kimoja) kupitia benki za **NMB, CRDB na NBC** au mitandao ya simu (**M-Pesa na Tigo Pesa**) kwa kutumia '**Control number**' itakayotolewa na NECTA.
- (d) Wasilisha fomu ya maombi NECTA ukiambatanisha cheti/hati ya matokeo iliyokosewa jina na stakabadhi ya malipo.

4.0 MAJIBU KWA MTEJA

- (a) Baada ya marekebisho kufanyika, Hati ya Matokeo (Results Slip) au cheti kipya chenye marekebisho kitatumwa kwa mkuu wa shule au kwa mtahiniwa (endapo si mwanafunzi).
- (b) Mtahiniwa ambaye atabainika kutokuwa na sifa ya kurekebishiwa jina, atajulishwa kwa barua kuwa marekebisho hayakufanyika kutokana na kutokuwa na sifa.